

Maswali

1. Nani walikuwa wakipigana na Wafilisti?
2. Nani alikuwa anakuja kutolea Mungu dhabihu na kuomba Mungu asaidie Waisraeli?
3. Mbona Sauli alitolea Mungu dhabihu?
4. Mbona Sauli hakutakiwa kutoa dhabihu?
5. Samweli alisema Mungu ataadhabi Sauli namna gani?
6. Mungu aliambia Samweli afanyeje Waamaleki ?
7. Sauli alitii amri za Mungu sawa sawa?
8. Sauli aliasi Mungu namna gani?
9. Sauli alipeana sababu gani?
10. Samweli alisema Mungu ataadhibu Sauli namna gani?

Majibu

1. Wafilisti walikuwa wakipigana na Waisraeli.
2. Samweli alikuwa anakuja kutolea Mungu dhabihu.
3. Samweli alikuwa amekawia kukuja na wanajeshi walikuwa wanatoroka.
4. Watu waliokuwa wamechaguliwa na Mungu ndio walitoa dhabihu.
5. Wana wa Sauli hawatakuwa wafalme baada yake. Mungu angechagua mfalme mwingine.
6. Mungu alimwambia Sauli aaribu Waamaleki wote na kila kitu chao.
7. Hapana.Sauli hakutii Mungu sawa sawa.
8. Sauli aliacha Agagi mfalme hai. Aliweka kondoo na ng'ombe wazuri.
9. Sauli aliweka kondoo na ng'ombe wazuri ili atolea Mungu
10. Samweli alisema kwa sababu Sauli alikuwa amekataa amri za Mungu, Mungu alikuwa amemkataa asiwe mfalme.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



58 Sauli anaasi Mungu

Kwa Biblia

1 Samweli mlango wa 13:5, mlango wa 14 na 15

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Sauli alimtumkia Mungu vizuri mwanzoni lakini pole pole aliharibiwa na ubinafsi na majivuno

Somo

Sauli hakuwa mfalme mzuri. Mungu alimchagua Sauli kuwa mfalme kwa sababu Waisraeli walitaka mfalme aliyekuwa mrefu, wa nguvu na hodari kwa vita. Mwanzoni Sauli alisikiliza Samweli tena alitii Mungu.

Sauli alikuwa na ubinafsi. Baada ya muda mfupi alikuwa mfalme wa majivuno. Halafu akaasi Mungu. Sauli hakufundisha Waisraeli wampende na wamtii Mungu. Alipoasi Mungu aliwaonyesha mfano mbaya. Kwa hili somo kuna njia mbili zenye Sauli aliasi Mungu.

Wafilisti walikuja kupigana na Waisraeli. Sauli alikusanya jeshi lake kuja kupigana nao. Wafilisti walikuwa wapiganaji hodari na silaha zao kali tena na magari yaendayo kwa kasi. Waisraeli wote waliogopa Wafilisti. Baadhi ya Waisraeli walitoroka, wengine walijificha kwa mapango, kwa mashimo, kwa misitu na hata kwa mwiamba. Wanaume wa jeshi la Sauli walitetemeka kwa hofu.

Samweli alikuwa amepanga kuja kwa kambi ya Sauli baada ya siku saba. Samweli angetolea Mungu sadaka ya kuteketezwa. Angeomba Mungu awasaidie Waisraeli kwa vita na Wafilisti. Dhabihu yoyote ilitolewa na watu waliochaguliwa na Mungu. Watu wengine wote hawakuruhuziwa kutolea Mungu dhabihu.

Sauli kwa siku saba aliongoja Samweli aje. Lakini Samweli alikawia. Sauli aliongoja, akangoja lakini Samweli hakukuja. Baadhi ya watu wa jeshi la Sauli waliogopa na kutoroka. Sauli hakusubiri. Hakuamini wala kutii Mungu. Sauli alichukuwa ndama wa kiume. Alitolea Mungu sadaka ya kuteketezwa kwa madhabahu.

Bunde tu Samweli aliwasili. Mungu aliudhika sana kwa uasi wa Sauli. Mungu alikasirika kwa sababu Sauli alitoa sadaka ya kuteketeza. Samweli aliuliza Sauli, "Umefanya nini?"

Sauli alikuwa na sababu tofauti tofauti, "Wafilisti walikuwa wanakuja kutupiga. Watu wangu wengine walikuwa wanatoroka. Wewe haukuja kwa wakati mzuri. Kwa hivyo MIMI MWENYEWE nilijitolea sadaka." Samweli alimwambia Sauli, "Umekuwa mpumbavu sana. Umemuasi Mungu. Kwa hivyo watoto wako hawatakuwa wafalme baada yako. Mungu atachagua mwingine kuwa mfalme baada yako." Samweli alipoondoka, Sauli alienda kwa vita kupigana.

Baada ya muda Mungu alituma Samweli kwa Sauli. Samweli aliambia Sauli, "Waamaleki walikuwa wabaya sana kwa Waisraeli huko jangwani. Amaleki ni taifa ovu sana. Mungu anataka uende uwapige kwa ajili ya huo uovu wao. Mungu anasema lazima uwe Waamaleki wote. Usiache yeyote atoroke. Uwaharibu wote. Tena lazima uharibu wanyama wote na kila kitu walichonacho uuwe."

Samweli aliambia Sauli, "Mungu anasema kwamba lazima uwauwe Waamaleki wote. Usiache yeyote atoroke. Lazima uwaharibu wote. Tena lazima uharibu wanyama wao wote na kila kitu chao."



Sauli alikusanya jeshi la Israeli lote. Waisraeli walishambulia Waamaleki. Sauli aliua Waamaleki wote isipokuwa mfalme. Sauli aliacha Agagi mfalme wa Amaleki hai. Tena Sauli aliacha kondoo na ng'ombe wazuri.

Samweli alienda kukutana na Sauli alipokuwa akirudi kutoka vitani. Sauli aliambia Samweli, "Nimefanya kila kitu vile Mungu aliamuru." Lakini Samweli alikasirika na kumuuliza, "Mlio wa kondoo na ng'ombe ninayosikia ni ya nini?" Sauli alibeanza sababu yake na kusema, "Tuliwaacha kondoo na ng'ombe waliowanono ili tumtolee Mungu sadaka lakini tukaua wale wengine wote."



Samweli alimwambia Sauli, "Umekuwa na majivuno. Hautii amri za Mungu. Unafikiri kwamba unafanya yaliyo mazuri. Unafanya kila kitu vile unataka sio vile Mungu anataka. Hakuna maana

kutoa maelfu ya sadaka za kuteketezwa na hali hautii amri za Mungu. Umemuasi Mungu. Umekataa kutii amri za Mungu. Kwa hivyo Mungu amekukataa wewe kuwa mfalme.

Samweli alipoondoka kwenda, Sauli alimshika joho ili amzuie. Joho ya Samweli iliraruka na kipande kilipaki kwa mkono wake. Samweli alimwambia, "Hivyo ni kama Mungu anararua ufalme kutoka kwako. Mungu atapeana ufalme kwa mtu mwingine."

Sauli aliasi Mungu. Kwa hivyo Mungu alinyang'anya Sauli na familia yake ufalme. Mungu alichagua mtu mwingine kuwa mfalme baada ya Sauli.